JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI

**WAKALA YA BARABARA TANZANIA**

Good roads for national development

30 Julai, 2026

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANROADS HAIVUMILII UKATILI; YACHUKUA HATUA BAADA YA TUKIO LA MIZANI YA KYAMYORWA**

Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) imesikitishwa na tukio la kushambuliwa kwa dereva, **Bw. Trabi Ayubu (48)**, mkazi wa Lushoto mkoani Tanga, lililotokea katika Kituo cha Mzani cha Kyamyorwa, Wilaya ya Muleba, Mkoa wa Kagera.

TANROADS inapenda kutoa ufafanuzi kuhusu mazingira ya tukio hilo pamoja na hatua zilizochukuliwa, huku ikisisitiza kuwa Wakala haukubaliani na hauvumilii matumizi ya nguvu au vitendo vya ukatili dhidi ya mwananchi yeyote katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mnamo tarehe **27 Julai, 2026**, majira ya saa **4:03 usiku**, gari lenye namba za usajili **T167 CCV**, aina ya Fuso, mali ya **Bw. Hizza A. Sheshe**, lililokuwa likitokea Geita kuelekea Mutukula likiwa limebeba mzigo wa mahindi, lilikaguliwa katika Kituo cha Mzani cha Kyamyorwa. Ukaguzi ulionesha kuwa gari hilo lilikuwa limezidisha uzito kwa **kilo 600 kwenye mtaimbo wa mbele (front axle)**, kinyume na masharti ya **Sheria ya Udhibiti wa Uzito wa Magari ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2016 (East African Community Vehicle Load Control Act, 2016) pamoja na Kanuni zake za mwaka 2018**.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, dereva alitakiwa kulipa faini ya **TSh 162,519.00** (Shilingi za Kitanzania laki moja sitini na mbili elfu mia tano na kumi na tisa).

Baada ya kufahamishwa kuhusu kiwango cha faini na kutakiwa kupeleka gari lake katika eneo la maegesho (yadi) kwa ajili ya malipo na kupanga upya mzigo uliozidi, dereva hakutekeleza maelekezo hayo na aliacha gari lake katika eneo la kupimia magari. Hali hiyo ilisababisha usumbufu wa utoaji huduma katika kituo hicho na kuzuia zoezi la ukaguzi wa magari mengine kwa takribani dakika 20.

Kutokana na hali hiyo, Afisa Mzani alijaribu kuwasiliana kwa simu na Mkuu wa Kituo Kidogo cha Polisi (OCS) Kyamyorwa ili kupata msaada wa kuondoa msongamano na kurejesha huduma. Baada ya kushindwa kumpata kwa wakati, aliomba msaada kutoka kwa walinzi wa kampuni ya **Nyamihaga Security Guard Limited**, ambao hulinda kituo hicho.

Ghorofa ya 3, 10 Makutano ya Mtaa wa Shaaban Robert Road na Garden Avenue, S.L.P 11364, Dar es Salaam,
Simu: +255222926001-6, Nukushi: +2552229211/2/3/4,
Barua pepe: tanroadshq@tanroads.go.tz, Tovuti: www.tanroads.go.tz

Baada ya dereva wa gari hilo kuendelea kukaidi kuliondoa katika eneo la mzani, baadhi ya walinzi hao waliamua kutumia nguvu dhidi ya dereva yaliyosababisha kushambuliwa na kupigwa.

**TANROADS inakemea vikali kitendo hicho.** Licha ya dereva kutotekeleza maelekezo yaliyokuwa yametolewa kwa mujibu wa sheria, hali hiyo haikutoa uhalali kwa mtu yeyote kutumia nguvu au kufanya shambulio la mwili dhidi yake. Vitendo vya aina hiyo ni kinyume cha sheria, maadili ya utumishi wa umma na taratibu za utoaji huduma za Serikali, na havina nafasi katika utekelezaji wa majukumu ya TANROADS.

Mara baada ya tukio hilo, TANROADS ilitoa taarifa kwa Mkuu wa Wilaya ya Muleba, ambaye baadae akiwa ameambatana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya alifika katika Kituo cha Mzani cha Kyamyorwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya awali ya tukio hilo.

Aidha, wahusika walielekezwa kuripoti katika Kituo cha Polisi kwa ajili ya uchunguzi, ambapo hatua za awali zilichukuliwa za kuwakamata na kuwashikilia watuhumiwa wanaodaiwa kuhusika ili uchunguzi ukamilike na hatua stahiki za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

Waliokamatwa kuhusiana na tukio hilo ni:

- **Bw. Kassim Ismaily Rweyongeza** – Afisa Mzani II, Kituo cha Mzani Kyamyorwa;
- **Bw. Lazaro Thomas** – Mlinzi wa Nyamihaga Security Guard Limited; na
- **Bw. Mohamed Ismail** – Mlinzi wa Nyamihaga Security Guard Limited.

Baada ya taratibu za kisheria kukamilika, dereva alilipa faini ya kiasi cha **TSh 162,519.00** mnamo majira ya saa **9:00 usiku** na kuendelea na safari yake kwa kuzingatia masharti ya sheria.

Aidha, TANROADS imeagiza kufanyika kwa mapitio ya kina ya taratibu za ulinzi na utoaji huduma katika Kituo cha Mzani cha Kyamyorwa pamoja na vituo vyote vya mizani nchini ili kuhakikisha matukio ya aina hii hayajitokezi tena. Wakala utaendelea kushirikiana kikamilifu na Jeshi la Polisi pamoja na vyombo vingine vya dola ili kuhakikisha uchunguzi unakamilika na hatua zote za kinidhamu na kisheria zinachukuliwa dhidi ya yeyote atakayebainika kuhusika, bila upendeleo.

TANROADS inapenda kuwahakikishia wananchi kuwa usalama, utu na haki za watumiaji wa barabara ni sehemu ya msingi wa utoaji huduma zake. Wakala umejipanga kuendelea kuboresha mifumo ya utoaji huduma katika vituo vya mizani ili kuhakikisha sheria zinatekelezwa kwa weledi, haki na heshima kwa kila mwananchi.

Wakati huo huo, TANROADS inawakumbusha madereva, wamiliki wa magari na watumiaji wote wa barabara kuzingatia sheria na kanuni za usalama barabarani pamoja na sheria za udhibiti wa uzito wa magari. Ushirikiano wa wadau wote katika kutii maelekezo yanayotolewa katika vituo vya mizani ni muhimu katika kulinda miundombinu ya barabara, kuimarisha usalama wa watumiaji wa barabara na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano Serikalini**
**Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS)**

Ghorofa ya 3, 10 Makutano ya Mtaa wa Shaaban Robert Road na Garden Avenue, S.L.P 11364, Dar es Salaam,
Simu: +255222926001-6, Nukushi: +2552229211/2/3/4,
Barua pepe: tanroadshq@tanroads.go.tz, Tovuti: www.tanroads.go.tz